

## **Mitanziko ya Wahusika katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi**

*Adria Fuluge*<sup>1</sup>

### **Ikisiri**

Watunzi wa kazi mbalimbali za fasihi huumba wahusika kwa ustadi mkubwa kwa lengo la kubeba maudhui na kuyafikisha kwa hadhira husika. Wahusika hao hubebeshwa fikra na tafakuri zinazoonisha hisia za mwandishi zinazoambatana na hali fulani katika kutoa maamuzi ya tafakuri yake. Miongoni mwa mambo hayo ni mitanziko ambayo hubainika kupitia matendo wafanyayo wahusika hao. Mitanziko hiyo husababisha wahusika kuchukua maamuzi ya kufanya au kutokufanya jambo fulani. Hivyo, makala hii inabainisha sababu za mitanziko ya wahusika katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974). Shabaha ya kubainisha sababu hizo kwa mwegamo wa kifasihi ni kuthibitisha kwamba fasihi ni zao la jamii na kwamba mitanziko inayowakumba wahusika katika riwaya hizo, ni usawiri wa wahusika halisi katika jamii, wanaokumbwa na mitanziko ya namna hiyo katika maisha yao ya kila siku. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini. Misingi miwili ya Nadharia ya Udhanaishi ilitumika katika uchunguzi, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya makala hii. Matokeo yanaonesha kwamba mitanziko inayowakumba wahusika katika riwaya teule inatokana na sababu kuu tatu, ambazo ni: za kijamii, kiutamaduni na kifalsafa.

### **1.0 Utangulizi**

Dhana ya mtanziko imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa namna tofautitofauti (Garofalo, 1981; Sletteboe, 1997; Madumulla, 2009). Mathalani, Sletteboe (1997) anafafanua kuwa mtanziko ni hali ya mhusika kuwa katika mkinzano wa mawazo ambao humpa wakati mgumu wa kuchagua jambo la kufanya kwa sababu uamuzi wowote anaoamua kuuchukua, huwa na madhara kwake. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, mtanziko husababishwa na matukio mabaya au ya hatari ambayo humkumba mhusika kiasi cha kumpa wakati mgumu wa kufikia maamuzi kuhusu jambo linalomtatiza. Kwa upande mwingine, Madumulla (2009) anaeleza kuwa mara nyingi mhusika akiwa katika mtanziko

---

<sup>1</sup> Mhadhiri, Idara ya Lugha na Stadi za Mawasiliano, Chuo Kikuu Mzumbe. Barua pepe: [adriafuluge@yahoo.com](mailto:adriafuluge@yahoo.com)

husukumwa katika ukingo wa kuamua kati ya kufa na kuyaepuka matatizo, au kuishi ili kuendelea na maisha kwa uvumilivu. Anafafanua zaidi kwamba kabla ya mhusika kuchukua maamuzi fulani hujiuliza maswali mbalimbali kuhusiana na mtanziko wake. Garofalo (1981) anaeleza kuwa mhusika huyo hufanya hivyo kwa sababu mtanziko ni suala la kisaikolojia linaloathiri fikra za mhusika ambazo humfanya atafakari kwa kina kuhusu jambo husika kabla ya kuchukua uamuzi wake. Ufafanuzi huo unaonesha kwamba ni vigumu kubainisha kwa uwazi sababu za mitanziko inayomkumba mhusika. Ndiyo maana katika jamii zetu, bado kuna matukio mengi yakiwamo ya watu kujiua ambayo huhusishwa na wahusika kupata mitanziko. Hivyo, kwa kuwa watunzi wa kazi za fasihi hutunga kazi zao kwa kuzingatia mambo mbalimbali yanayosawiriwa katika jamii, makala hii inalenga kujadili sababu za mitanziko ya wahusika zinazosawiriwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974).

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala hii imetumia Nadharia ya Udhanaishi katika kuchunguza, kujadili na kuwasilisha data zinazohusu mitanziko ya wahusika katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974). Wamitila (2003) anaeleza kuwa udhanaishi ni mtazamo unaohusiana na hali na maisha ya binadamu, nafasi na majukumu yake ulimwenguni na uhusiano wake na Mungu. Nao Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba udhanaishi ni falsafa inayotokana na ‘utamaushi,’ yaani kutokuwa na furaha na kukosa tumaini katika maisha. Kwa mujibu wa Mulokozi (1983), Diegner (2002) na Wamitila (2003), Nadharia ya Udhanaishi inatokana na mawazo ya Soren Kierkegaard (1813 - 1855). Wataalamu hao wanafafanua kwamba katika vitabu vyake vya *Fear and Trembling* (1843), *The Concept of Dread* (1844) na *Sickness unto Death* (1849), Kierkegaard anaeleza kwamba mtu ni kikaragosi cha nguvu zilizomuumba na za kijamii. Aidha, mtu huyo hupata kimbilio kutoka katika mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu.

Nadharia hii iliendelezwa na wataalamu wengine katika karne ya ishirini wakiwamo Friedrich Nietzsche (1844 – 1900), Gabriel Marcel (1889 – 1973), Martin Heidegger (1889 – 1976) na Albert Camus (1913 – 1960). Katika maelezo yake kuhusu udhanaishi, Camus (1984) anasema kuwa udhanaishi ni falsafa inayoshughulikia masuala mbalimbali ya maisha. Anafafanua zaidi kwamba madhumuni ya maisha siyo kuishi kwa furaha bali kufa ukiwa mwenye furaha. Camus anaugawa Udhanaishi katika miegamo miwili: Mosi, maisha kama ombwe, yaani mahali patupu, na kwamba maisha yenyewe hayana maana. Pili, kujiua kama suluhisho la matatizo anayokabiliana nayo binadamu, na kuamini kwamba hakuna

maisha baada ya kifo. Kwa ujumla, wadhanaishi huyaona maisha ya mtu kuwa ni ya kitanzia na kwamba hayana maana kwa kuwa mwisho wa mwanadamu ni kifo (Camus, 1984; Wafula na Njogu, 2007).

Hivyo, uandishi wa makala hii umejikita zaidi katika mihimili miwili ya udhanaishi kulingana na mawazo ya jumla ya wadhanaishi. Mosi, kutafuta uhuru binafsi. Pili, kukata tamaa katika maisha. Mihimili hii imetuongoza katika kujadili sababu za mitanziko ya wahusika inayosawiriwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974).

### **3.0 Methodolojia**

Ukusanyaji, uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo ya makala hii vilitumia mkabala wa kitaamuli. Data zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usomaji na uchambuzi wa riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974). Riwaya hizo ziliteuliwa kwa sababu zina mawanda ya kutosha yaliyotwezesha kupata data zilizolengwa katika makala hii. Aidha, mtafiti alisoma maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya makala yake yakiwamo majarida, vitabu na magazeti ili kushadidia data zilizopatikana katika riwaya teule. Misingi ya Nadharia ya Udhanaishi ilimwongoza mwandishi wa makala katika kujadili na kupatikana kwa matokeo ya utafiti huu.

### **4.0 Matokeo ya Utafiti**

Baada ya kusoma na kuchambua kwa makini riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974), tumebaini kwamba wahusika katika riwaya hizo wamekumbwa na mitanziko tofautitofauti. Aidha, tumebaini kuwa zipo sababu mbalimbali zinazochangia wahusika hao kukumbwa na mitanziko hiyo. Hivyo, makala hii inajadili sababu kuu tatu, ambazo ni: za kijamii, kiutamaduni na kifalsafa.

#### **4.1 Sababu za Kijamii**

Wataalamu mbalimbali kama vile Wellek na Warren (1949) na Escarpit (1974)) wanaeleza kwamba uhusiano baina ya fasihi na jamii husawiriwa kwa kuchunguza namna kazi husika inavyofungamana na jamii. Wanafafanua zaidi kuwa uhusiano huo huenda sambamba na mabadiliko ya jamii katika nyanja mbalimbali. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kuzichunguza kazi za fasihi kama zao la jamii ambalo pia huweza kuathiri na kuathiriwa na jamii husika. Hivyo, kwa kuwa fasihi huwakilisha maisha (Mulokozi, 2017), sehemu hii inajadili baadhi ya sababu zenye uhusiano wa moja kwa moja na maisha halisi ya jamii. Sababu hizo ni mfumo wa malezi na uhusiano wa kimapenzi.

#### 4.1.1 Mfumo wa Malezi

Malezi ni mchakato wa ukuzaji wa mtu tangu umri wa utotoni hadi utu uzima kwa kuhusisha wanaohusika na malezi, mazingira, wakati na mfumo wa jamii husika (Green, 2007). Katika kujenga jamii imara na inayozingatia maadili mema, suala la malezi ni muhimu na linapaswa kuzingatiwa na kila mtu katika jamii (Ogundipe-Leslie, 1984; Ndungo, 1998; Mbatiah, 1998). Mathalani, Ndungo (1998) asema kuwa malezi huchukua nafasi muhimu katika kuunda na kuimarisha itikadi na mielekeo ya jamii husika. Umuhimu huo unatokana na ukweli kwamba malezi ni mchakato wa kumtunza na kumsaidia mtoto, tangu kuzaliwa hadi utu uzima, kwa kuhusisha maumbile, hisia, jamii na uwezo wa kiakili (Fuluge, 2021). Mchakato huo hulenga kumkuza na kumfundisha mtoto kabla au baada ya kuzaliwa hadi anapofikia umri wa utu uzima, ili kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Ogundipe-Leslie (1984) anaeleza kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika, mfumo wa malezi hupitia michakato mbalimbali. Pia, mifumo hiyo humtoa mhusika katika hali ya utoto na kuwa mtu mzima. Anafafanua zaidi kwamba wazazi na walezi huhakikisha kuwa mtoto anaandaliwa mapema na kutambua mambo yote muhimu kama binadamu mkamilifu. Hata hivyo, katika riwaya teule mwandishi anaonesha ugumu uliopo katika malezi ya watoto, hususani wa kike. Anaona kuwa malezi ayapatayo mtoto mdogo, huwa na athari kubwa katika maisha yake ya baadaye. Anabainisha kuwa wazazi au walezi wanapotofautiana katika misimamo ya namna ya kuwalea watoto wao, huwaweka watoto hao kwenye mitanziko ya maisha yao ya baadaye kama inavyojitokeza katika riwaya hizo.

Kwa mfano, katika riwaya ya *Rosa Mistika* tumbaine kuwa malezi aliyopata Rosa kutoka kwa wazazi wake, hususani kwa Zakaria, yanamsababishia mtanziko katika maisha yake kama inavyothibitishwa na mwandishi katika nukuu inayosema:

Hivi ndivyo Rosa alivyolelewa; hivyo ndivyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa na baba yake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote. Na Zakaria alipojua hayo alifurahi sana. Alijidai kwamba yeye alifahamu jinsi ya kulea binti zake – hasa alipokuwa amekunywa kidogo. Hakufahamu kuwa Rosa alikuwa katika rika baya, na kwamba ukali ulikuwa haufai; hakufahamu kuwa mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao; hakufahamu kwamba kwa kumpiga bintiye alikuwa akiingilia utawala usio wake, na kwamba kuhusu maoni ya ndoa yake alifahamu kidogo sana; na hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana. Kwa hiyo, kutokana na malezi ya namna hii, Rosa alianza kuwaangalia wavulana kama watu wasiopaswa kuandamana nao, au hata kuzungumza nao (Kezilahabi, 1971: 9).

Dondoo hili linaonesha kuwa malezi ya kunyimwa uhuru, ukali, vitisho na ukatili wa Zakaria dhidi ya binti yake, ndiyo yanayojenga chuki na uhasama baina yao. Musau (1995) anaeleza kwamba Zakaria anaamini kuwa hayo ni malezi bora ambayo ufanisi wake utaonekana pale binti huyo atakapomletea mahari, baada ya kuolewa. Hata hivyo, makala hii imebaini kwamba malezi ya namna hiyo yanakuwa sababu ya Rosa kutofahamu namna ya kukabiliana na matatizo yanayotokana na maisha ya kisasa nje ya kijiji chao, na mbali na jicho la baba yake. Matokeo yake, akiwa katika shule ya Sekondari ya Rosary, anapata mtanziko kwani analazimika kuchagua ama kuendelea kufuata misingi ya malezi aliyopewa na wazazi wake au kwenda kinyume. Matokeo yanaonesha kwamba Rosa anaamua kukiuka misingi ya malezi aliyopewa. Kimsingi, Rosa anafanya hivyo kuwakilisha vijana wengi katika jamii, ambao maisha yao yameathiriwa na mifumo ya malezi yanayowanyima uhuru kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi.

#### **4.1.2 Uhusiano wa Kimapenzi**

Tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba uhusiano wa kimapenzi ni sababu mojawapo inayochangia watu wengi kupata mitanziko (Sabinus, 2018; WHO, 2018; Fuluge, 2021). Kwa mujibu wa WHO (2018), hali hii huwapata zaidi vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 29, ambapo wengi wao hujaribu kufanya mambo mengi ili kufikia matarajio yao. Hata hivyo, inapotokea kuwa matarajio hayo hayakufikiwa, huweza kukumbwa na msongo wa mawazo, na hivyo, kujikuta katika hali ya mtanziko. Ithibati ya maelezo haya inatolewa na Sabinus (2018) anapoeleza kuwa miongoni mwa sababu za watu kupata mitanziko na hata wengine kufikia maamuzi ya kujiua ni msongo wa mawazo unaotokana na uhusiano wa kimapenzi.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* suala la uhusiano wa kimapenzi linajitokeza na kusababisha mitanziko miongoni mwa wahusika akiwamo Rosa Mistika. Mhusika huyu anajikuta katika mtanziko wa uhusiano wa kimapenzi na watu mbalimbali akiwamo Charles, Deogratias na Bwana Thomas. Katika makala hii imebainika kwamba Rosa akiwa darasa la sita, anapata mtanziko mara tu baada ya kuandikiwa barua ya mapenzi na Charles.

Barua hii fupi imebeba ujumbe unaoibua na kuchochea hisia, msisimko na fikra nzito ndani ya moyo wa Rosa Mistika, zinazomwingiza katika uhusiano wa kimapenzi na Charles. Hata hivyo, uhusiano wenyewe haudumu, kwani unaingia dosari baada ya Zakaria, baba yake Rosa, kupata taarifa kuhusiana na barua hiyo na kuamua kumshushia kipigo kizito. Kipigo hicho kinamsababishia Rosa mtanziko, ambapo kama asemavyo Kipacha (2019), Rosa anatakiwa kuchagua ama kukubaliana na kutii sheria ngumu, kali, kandamizi na zinazomnyima uhuru kutoka

kwa baba yake au kuzitupilia mbali na kuendelea na uhusiano wa kimapenzi na Charles. Makala imebaini kwamba kukosekana kwa uhuru wa kujiamulia mambo yake mwenyewe kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi kunamkatisha tamaa na kumsababishia woga katika maisha yake.

Vilevile, utafiti umebaini kwamba Rosa anapata mitanziko zaidi anapotoka katika malezi na sheria za kunyimwa uhuru kutoka kwa Zakaria. Hii ni kwa sababu anakumbana na sheria nyingine ngumu zaidi za masista katika shule ya Sekondari ya Rosary. Sheria hizo zinamweka katika mtanziko kwani zinamkosesha uhuru wa kujiamulia mambo yake mwenyewe kama kiumbe razini na hivyo kulazimika ama kuendelea kuishi kwa kuzingatia sheria hizo au kuachana nazo na kuishi kwa uhuru kulingana na matakwa yake. Matokeo yanaonesha kwamba uvumilivu wake wa kuendelea kufungwa katika minyororo hiyo ya ukandamizaji unamwishia na kuamua kujitafutia uhuru binafsi kwa kufanya mambo kulingana na utashi wake. Hivyo, anaanza kuiga tabia za wasichana wenzake; anaamua kutoroka usiku kwenda kucheza dansi. Anapata msukumo huo baada ya kuumizwa na maneno ya wanafunzi wenzake. Anajiuliza:

‘Huyu John ni nani? Wanasema kwamba mimi kilema! Nimekosa nini? Walikuwa wanamaanisha nini waliposema kwamba mimi kilema. Wanasema baba mkali. Kuna ubaya gani! Si ananilinda!’ Hata alipokuwa kitandani maneno haya yaliendelea kuzunguka kichwani mwake. Alikata shauri kwenda kucheza dansi (Kezilahabi, 1971: 30).

Katika nukuu hiyo Rosa anapata mtanziko kutokana na kauli za wanafunzi wenzake kumwita kilema ilhali yeye anajiona yu mzima. Kitendo hicho kinamwingiza katika tafakuri nzito kiasi cha kushindwa hata kupata usingizi. Takafuri hiyo inamfanya ajiulize maswali yanayomsukuma katika kuasi misingi ya malezi aliyoyapata kutoka kwa baba yake. Anasema:

Kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yuko Ukerewe, mimi niko Usukuma, baba anakaa akinichunga anafikiri atania? (Kezilahabi, 1971: 32).

Maoni yetu kutokana na nukuu hii ni kuwa kitendo cha Rosa kujiingiza na kuanza mapenzi kwa madai kwamba baba yake yuko mbali na hamwoni, kinamweka katika mtanziko zaidi anapotambua kwamba kunyimwa uhuru huko kumemchelewesha kufanya mambo mbalimbali. Hivyo, anaamua kujiingiza katika bahari ya mapenzi kwa pupa, pasipo kufanya maandalizi ya kutosha. Tabia na mwenendo wake sasa vinatawaliwa na kukumbwa na nguvu ya mazingira yake mapya, tofauti na yale aliyoyazoea. Mbatiah (1998) anaeleza kuwa Rosa anaamua kutumbukia katika

bahari iliyochafuka ya mapenzi bila kujua kuogelea. Mwandishi anathibitisha akisema:

Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huohuo aliwakubalia wavulana watano (Kezilahabi, 1971: 33).

Kutokana na dondoo hili tumebaini kwamba uhuru anaojitafutia anautumia vibaya na unamzamisha katika bahari ya mapenzi ambayo haimalizi kiu yake. Matokeo yake anapata mtanziko kwani anashindwa kufanya uamuzi wa kuchagua mwanamume sahihi wa kuwa naye katika uhusiano wa kimapenzi, badala yake anakuwa na wanaume wengi kwa wakati mmoja. Yote hayo ni kutokana na mabadiliko ya tabia yake kama asemavyo Kipacha:

Rosa anaamua kubadilika kitabia baada ya wanafunzi wenzake kumtusi na kumwita kilema kwa kukataa vishawishi vya kujiingiza katika tabia ya ufuska. Hata hivyo, anapoamua kuendana na tabia za wanajamii waliomzunguka, anatumbukia katika mtego wa kushutumiwa kwa tabia yake ya ufuska na ulevi kupindukia. Rosa anapitia kipindi cha utambuzi kuwa, mifumo ya uthamani ya kitamaduni na kimaadili inayomzunguka haina mantiki wala haimsaidii; na yote ni ya kidanganyifu. Hivyo, anaamua kuitupilia mbali na kuchukua mkondo wake kwa kukataa minyororo iliyokuwa ikimfunga kama msichana, mwanamke na mwanajamii (Kipacha, 2019: 423 - 424).

Aidha, imebainika kwamba kutokana na kuendekeza tabia yake ya umalaya, Rosa anapata mtanziko wa uhusiano wa kimapenzi akiwa Chuo cha Ualimu Morogoro. Huko pia, anajiingiza katika mahusino ya kimapenzi na watu wengi, akiwamo Mkuu wa Chuo hicho, Bwana Thomas. Matokeo yake, anazidi kupatwa na masaibu baada ya kufumaniwa na mke wa mwalimu huyo ndani ya nyumba yake, wakiwa katika ulimwengu wa mapenzi. Mwandishi anasema:

Mara moja mke wa mwalimu aliingia na shoka lake mkononi limeinuliwa juu tayari kumwangukia Rosa kichwani. Mwalimu alilidaka hewani. "Leo utanitambua! Unataka kuniletea hapa umalaya wako!" Rosa alijaribu kukimbia. Alishikwa na yule mwanamke. Rosa alianguhwa chini. Yule mwanamke alimwinamia. Rosa alitiwa jino. Palepale uso wa Rosa ulienea damu (Kezilahabi, 1971: 54).

Kinachodhihirika katika dondoo hilo ni kwamba Rosa yuko katika mtanziko, kwani anashindwa kujua la kufanya kutokana na mazingira magumu ya kufumaniwa anayokumbana nayo. Tukio hilo linazidi kumsogeza katika mtanziko zaidi anapoona kuwa thamani yake inazidi kupungua baada ya kuumizwa na mwanamke

huyo kwa kukatwa sikio lake. Kipacha (*keshatajwa*) anaeleza kuwa tukio hili linamweka Rosa katika njiapanda katika kuishi duniani; hivyo, anafikiria kujiondoa duniani (uk. 431). Maelezo haya yanathibitisha kuwa mhusika huyu yuko katika mtanziko.

Vilevile, katika riwaya ya *Kichwamaji*, utafiti umebaini kuwapo kwa mtanziko wa uhusiano wa kimapenzi kwa wahusika wengine ambao ni Rukia, Kazimoto na Manase. Kwa upande wa Kazimoto, imebainika kwamba mhusika huyu anakumbwa na mtanziko unaotokana na uhusiano wa kimapenzi baina yake na Pili, ambapo kutokana na uhusiano huo, Pili anamwambukiza Kazimoto ugonjwa wa ajabu. Mwandishi anaeleza:

... ugonjwa huo ulikuwa hauwezi kutambulika kwa urahisi. Ugonjwa huo unaingia ndani ya damu na kukaa bila kumdhuru mhusika. Baada ya miaka kumi na minne hivi au zaidi unanza kumdhuru mhusika, lakini kabla yake ni vigumu kuusikia (Kezilahabi, 1974: 192).

Matokeo yanaonesha kwamba Kazimoto aliambukizwa ugonjwa wa zinaa kutoka kwa Pili kutokana na umalaya wa msichana huyu. Kwa upande mwingine, Kazimoto naye, kutokana na umalaya wake, anamwambukiza mke wake, Sabina. Madhara ya ugonjwa huo ni Sabina kuzaa mtoto mwenye kichwa kikubwa na kuleta mgogoro baina yake na Kazimoto. Hatimaye, mgogoro huo unasababisha mtanziko kwa Kazimoto kiasi cha kuona kwamba hakuna haja ya kuendelea kuishi. Hivyo, anaamua kujiua baada ya kutanzikwa na suala hilo kama anavyothibitisha mwandishi wa riwaya hii anaposema: “Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya.” (uk. 195).

Kimsingi, kauli ya Kazimoto kwamba amejiua kwa sababu hataki kuendelea kuzaa kizazi kibaya inathibitisha kwamba, kabla ya kufikia uamuzi huo alikuwa katika mtanziko na kwamba alitakiwa kuamua kati ya mambo mawili, ama kufa au kuendelea kuishi. Camus (1984) anaipambanua falsafa ya kujiua katika *The Myth of Sisyphus* (1942), ambapo mwanadamu kama inavyothibitika kwa Kazimoto, yumo katika njiapanda pale anapoishi duniani; ama aamue kujiondoa duniani au aamue kuishi katika dunia yenye kukatisha tamaa. Hivyo, Kazimoto anaamua kujiua baada ya mtanziko huu kama inavyothibitika kupitia mazungumzo baina yake na Sabina:

“Mke wangu,” nilimwita.

“Bwanangu,” aliitikia.

“Sijui kwa nini ninaishi.”

“Nimechoka na maswali yako ya kijinga,” alisema.

“Huwezi kuishi kama watu wengine?” Wewe nani?”

“Mimi sijijui,” nilimwambia (Kezilahabi, 1974: 194 - 195).



Majadiliano haya yanaonesha kuwa Kazimoto yuko katika mtanziko na amekata tamaa ya kuishi. Tunathibitisha hoja hii kutokana na maneno yake anaposema hajui kwa nini anaishi na kwamba hajijui. Bila shaka anatoa majibu hayo akiwa katika mtanziko na hajui afanye nini kutokana na matatizo anayoyapitia. Aidha, majibu ya Sabina kwamba amechoshwa na maswali ya Kazimoto ni ithibati nyingine kwamba suala hili limempa wakati mgumu Kazimoto na anafikia uamuzi huo baada ya kuyatafakari kwa kina matatizo yanayomkabili. Kama inavyoeleza Nadharia ya Udhanaishi, anaonekana amekata tamaa ya maisha. Hatimayae, anaamua kujua kama suluhisho la matatizo anayopitia.

#### **4.2 Sababu za Kiutamaduni**

Utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu fulani unaohusisha michakato ya kijamii ambayo huiwezesha jamii hiyo kujielezea na kujitambulisha, pamoja na kufanya shughuli za kila siku (Wizara ya Elimu na Utamaduni, 1997; Wamitila, 2006; Khamis, 2007). Katika ufafanuzi wake, Khamis (2007) anaeleza kuwa utamaduni ni maisha ya mtu au jamii katika mazingira maalumu ya asili yanayojumuisha lugha mama, imani, mila, maadili, itikadi, desturi, sanaa, michezo na kazi zao mahususi. Nayo Wizara ya Elimu na Utamaduni (1997) inaeleza kuwa utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Ufafanuzi huo unamaanisha kwamba utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wa mambo na taratibu za jamii katika kuendesha maisha yake. Katika makala hii imebainika kuwa, miongoni mwa vipengele vya utamaduni wa Kiafrika vinavyoweza kusababisha mitanziko kwa wahusika ni: masuala ya mila na desturi, dini na tatizo la ndoa na uzazi. Vipengele hivi vimejadiliwa kama ifuatavyo:

##### **4.2.1 Mila na Desturi**

Waafrika wanaamini katika mila na desturi zao ambazo hujidhihirisha kwa njia mbalimbali kama vile: vyakula, utoaji majina, dini, nyimbo na ngoma zao (Mbiti, 1969). Vipengele vya mila na desturi vimejadiliwa katika sehemu hii kwa namna mbili, yaani urithi wa mali na ulipaji wa mahari. Kwa mujibu wa BAKITA (2017), urithi ni mali na vitu vingine vyote vilivyoachwa na mtu aliyefariki dunia ili vigawiwe kwa wanawe na ndugu zake wa karibu. Sambamba na fasili hiyo, Swai (2021) anaeleza kwamba mtu anaweza kugawa mali alizonazo kwa ndugu zake kwa ridhaa yake kabla hajakutwa na umauti. Kuhusiana na suala la urithi wa mali za marehemu, katika makala hii tumebaini kwamba ugawanyaji wa mali usiozingatia usawa na miongozo sahihi, huweza kusababisha mitanziko na mafarakano katika

jamii. Jambo hili linasawiriwa katika riwaya ya *Rosa Mistika*, kwani ndugu wa Zakaria wanaamua kugawana mali zake mara tu baada ya kifo chake. Wanaukataa ujumbe ulioachwa na Zakaria kwamba warithi wa mali zake ni watoto wake. Badala yake, ndugu hao wanagawana mali hizo pasipo kuwashirikisha watoto wa Zakaria. Mwandishi anasema:

Kijikaratasi kilisema kwamba warithi walikuwa ni watoto tu. Kila mtoto alikuwa amepangiwa vitu vya kurithi. ... Hawa jamaa, kweli walirithi. Lakini hapakuwa na mtu mmoja aliyeweza kusema atamchukua mtoto fulani amtunze (Kezilahabi, 1971: 96).

Data hiyo inaonesha namna jamaa wa Zakaria walivyorithi mali na kuwaacha watoto wake katika mtanziko. Imethibitika kwamba, licha ya Zakaria kuacha wosia kuhusu warithi wa mali zake, ndugu hao wanaukataa na kuendelea na mchakato wa kugawana mali bila kuwashirikisha. Matokeo yake watoto wanaachwa katika mtanziko wasijue namna watakavyoishi, kwani hakuna hata mmoja wao anayetaka wajaadili namna ya kuwalea.

Suala jingine linalosawiriwa na mwandishi ni ulipaji wa mahari. Kulingana na mila na desturi nyingi za Kiafrika, mtoto wa kike kabla ya kuolewa, hulazimika kulipiwa mahari, inayohusisha vitu mbalimbali kama vile wanyama, vifaa vya kazi, pamoja na fedha. Tukio la ulipaji mahari huhusisha watu teule wa ukoo ambao hushiriki na kuamua kiwango cha mahari inayoafikiwa (Reed, 2009). Kimsingi, kitendo cha kulipa mahari ndicho huhalalisha ndoa yoyote itakayofungwa. Hata hivyo, tendo hili lisipofanyika kwa uangalifu, huweza kusababisha mitanziko kwa wahusika.

Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji*, mwandishi anaonesha namna mahari inavyosababisha mtanziko katika familia ya Mzee Mafuru. Hii ni baada ya familia ya Kabenga kuipangia familia ya Mafuru kiasi kikubwa cha mahari. Mazungumzo baina ya Kazimoto na Sabina yanathibitisha suala hili:

Baba yako amedai mahari ambayo nilikuwa sijapata kusikia. Baba pia mkaidi. Amesema hata kama ninaweza kutoa, hawezi kuniruhusu nitoe na nikuo wewe kwa mahari kama hayo, kama kwamba kuna uadui kati yetu na ninyi (Kezilahabi, 1974: 142 - 143).

Kinachobainika katika dondoo hilo ni kwamba suala la ulipaji wa mahari linawapa mtanziko Kazimoto na Sabina kwa sababu Mzee Mafuru hayuko tayari kulipa mahari hiyo, licha ya kuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Msimamo wa Mzee Mafuru unamweka Kazimoto katika mtanziko kwani hajui afuate ama uamuzi wa baba yake au achukue uamuzi tofauti. Kwa upande wake, Sabina anapata mtanziko kwa kuhofia kumkosa mchumba wake, Kazimoto, kama atakubaliana na maoni ya baba

yake kwamba wasilipe mahari hiyo. Katika majadiliano yake na Kazimoto, Sabina haoni sababu ya baba yake kudai mahari kubwa, kwani haipaswi kufanywa kama kitegauchumi kwa wazazi wa mtoto wa kike.

“Baba ameomba kiasi gani?”

“Ameomba shilingi elfu moja; ng’ombe watatu, dume na jike wawili; mbuzi watano; visu vinne, kinu, nafikiri vilevile na mchi wake, na kitanda.”

“Kweli, baba hawezi kudai hayo yote kama kwamba ananiuza. Kwani anafikiri anaweza kutajirika siku moja! Mahari ni mazuri lakini lazima yakadiriwe. Mahari yanapoteza maana kama wazazi wakianza kupata wazo la faida vichwani mwao...” (Kezilahabi, 1974: 142 - 143).

Kinachothibitika katika majadiliano haya ni kwamba Kazimoto na Sabina wako katika mtanziko wa kuoana unaotokana na Kabenga kupanga mahari kubwa. Matheru (1982) anaeleza kwamba mahari inapotolewa inamfunga mwanamke kwa mumewe, na kwamba, hata akiteswa anavumilia kwa sababu akitoroka wazazi watapaswa kurudisha mahari. Kwa mujibu wa makala hii, ulipaji wa mahari ni suala muhimu katika kukuza na kuendeleza mila na desturi za jamii husika. Hata hivyo, suala hili linatakiwa kufanyika kwa tahadhari kubwa, kwani lisipoendeshwa vizuri, huweza kusababisha mitanziko kwa wahusika na kuwakatisha tamaa ya maisha kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi.

#### 4.2.2 Dini

Dini ni mfumo wa imani wa kuabudu na kuheshimu Muumba (Idowu, 1973). Kulingana na mtaalamu huyu, dini hutawala mfumo wa maisha ya mtu katika idara zake, kwa kuwa humwekea misingi muhimu ya maisha. Mbiti (1969) anaeleza kwamba dini ina nguvu kubwa kuliko asasi nyingine za kiitikadi, kwa sababu huathiri fikra za watu. Anaongeza:

Dini za asili zinachukua nafasi katika kila nyanja ya maisha, hakuna tofauti rasmi kati ya mfumo wa dini na ule usio wa dini, kati ya maisha ya kiroho na yasiyo ya kiroho. Popote alipo Mwafrika, kuna dini yake: anaipoleka shambani katika kupanda au kuvuna... na kama akiwa ameelimika, anaipoleka dini kwenye chumba cha mtihani shuleni au chuoni; akiwa ni mwanasiasa ataipoleka dini bungeni (Mbiti, 1969: 2).

Kwa maelezo hayo, Mbiti anaonesha kuwa pamoja na ujio wa dini za Kikristo na Kiislamu, Waafrika wamezungukwa na dini zao za jadi. Naye Awolalu (1976), anaeleza:

... tunapozungumzia dini za jadi ya Kiafrika tunamaanisha imani na desturi ya dini ya asili ya Waafrika. Ni dini ambayo inatokana na kushikilia imani za mababu wa Waafrika wa leo, na inayoabudiwa nyakati hizi kwa namna na vivuli tofauti vya uzito, na idadi kubwa ya Waafrika, wakiwamo wale wanaodai kuwa ni Waislamu au Wakristo (Awolalu, 1976).

Dondoo hili linaonesha kwamba Waafrika huamini katika miungu yao, na kwamba jambo fulani likitokea vinginevyo hutazamwa kama laana. Kutokana na hilo, kama asemavyo Mbiti (*keshatajwa*), wengi wao wanapokumbwa na majanga mazito hukimbilia ama katika dini zao za jadi au dini za kigeni kwa imani kuwa hii ndiyo asasi yenye ulinzi kamili. Hata hivyo, makala inaonesha kuwa dini huweza kumsababishia mhusika mtanziko, hasa anaposhikilia sana misingi ya imani yake na kuibua mitazamo inayokinzana na jamii yake.

Suala hili linathibitika katika riwaya ya *Kichwamaji* na linasababisha mtanziko kwa Sabina. Linamfanya aonekane tofauti kulingana na mitazamo ya jamii yake. Hilo linatokana na msimamo wake wa kushikilia sana misingi ya dini ya Uprotestanti kama asemavyo mwandishi:

Sabina alikuwa anaogopwa na vijana wengi kutokana na msimamo wake kwa kuwa alikuwa Mprotestanti halisi. Dini ilimkaa sana moyoni. Wale waliomnyemelea aliwajibu kwa misemo ya Biblia. “Msichana mcha Mungu huyo utamwezaje?” Vijana walijiuliza (Kezilahabi, 1974: 101).

Katika data hiyo, mwandishi anaonesha namna dini inavyomtenga Sabina na jamii yake kutokana na msimamo wake wa kushikilia misingi ya dini kiasi cha kuogopwa na vijana wenzake. Mtanziko huo unamkoshesha mtu wa kumwoa kwa sababu vijana wenzake wanatilia mkazo majibu aliyozoea kuyatoa kuhusu msimamo wake wa dini. Mazungumzo baina yake na Kazimoto ni ithibati ya hoja hii:

“Kazimoto,” alianza kuzungumza. “Kama ungefahamu taabu ambazo nimekwishapata usingeniambia vile. Mimi nimo katika huzuni. Usifikiri kwamba mimi sipendi kuolewa au kwamba sipendi wanaume. Kazimoto, ni vigumu kupata wanaume (Kezilahabi, 1974: 101).

Msimamo wa Sabina kuhusu dini yake, ndio unaomsababishia mtanziko. Hilo linathibitika kupitia kauli yake kwamba yuko katika huzuni kwa sababu ya ugumu wa kuwapata wanaume wa kumwoa.

#### 4.2.3 Ndoa na Uzazi

Katika jamii nyingi za Kiafrika, uzazi huthaminiwa sana kwa sababu mtoto huonekana kuwa ni baraka kutoka kwa miungu au Mungu (Mbiti, 1969; Kajosi,

2013; Chuachua, 2016). Baraka hizi zina umuhimu kwa wazazi na jamii. Hata hivyo, ndoa nyingi hukumbwa na migogoro kutokana na sababu mbalimbali likiwamo suala la uzazi. Chuachua (*keshatajwa*) anasema kwamba kwa kawaida, minong'ono huanza baada ya mwaka mmoja au miezi michache tu tangu kufunga ndoa, endapo hakuna dalili za kupatikana kwa mtoto (uk. 231). Migogoro ya ndoa na matatizo ya uzazi husababisha mitanziko katika jamii, hususani wahusika wanaposhindwa au kukosa uwezo wa kuzaa au kupata watoto wa jinsia fulani tu. Katika jamii nyingi za Kiafrika, heshima ya ndoa hukamilika wanandoa wanapopata watoto, hususani wa kiume (Lugano, 1989 na Kimani, 2003). Kimsingi, kwa Waafrika, thamani ya mwanamke hutokana na uwezo wake wa kuzaa watoto wengi (Temples, 1959; Lugano, 1989; Mbiti, 2011). Hii ni kwa sababu watoto huchukuliwa kama baraka katika jamii. Hivyo, mwanamke wa Kiafrika anaposhindwa kupata mimba au kuzaa watoto wa jinsi moja tu, ndiye huelekezewa lawama zote hata kama tatizo hilo husababishwa na mwanamume. Mbiti (1969) anathibitisha hili anaposema:

... kwa hiyo ni jukumu la kidini na kijamii, kwa kila mmoja kuo au kuolewa; na kama mwanamume hana mtoto au ana watoto wa kike pekee, atafute mke mwingine, ili kupitia kwake, watoto wa kiume waweze kuzaliwa, ambao wataendeleza ukoo wake na kumweka pamoja na wafu wengine katika familia (Mbiti, 1969: 26).

Maelezo haya yanaonesha kwamba ndoa haiwezi kukamilika kama mwanamke hatakuwa na uwezo wa kuzaa. Mtazamo wa Mbiti kama ilivyo kwa Waafrika wengi, unathibitisha kuwa tatizo la kutozaa au kuzaa watoto wa jinsi moja tu, husababishwa na mwanamke. Faustine (2017) anashadidia hoja hiyo anaposema, katika jamii za Kiafrika wanandoa wasiobahatika kupata watoto, huwa hawathaminiwi. Vilevile, ndoa zao, mara nyingi, huwa hazidumu; au mwanamume huamua kuo au mke mwingine ili kumzalika watoto. Hilo linajitokeza kwa Regina katika riwaya ya *Rosa Mistika*, kwani Zakaria anakusudia kumwacha kwa sababu ya kuzaa watoto wa kike pekee. Mwandishi anasema:

Lakini Regina tangu aolewe hakuwa na raha: alikuwa akisumbuliwa na kuteswa na mumewe kwa kosa lisilo lake. Regina alikuwa na watoto watano wasichana; wote wazuri kama yeye. Matumaini yake ya kukaa pamoja na watoto hao kama alivyoambiwa na bwanake yalika katika mimba ya miezi mitano aliyokuwa nayo sasa... (Kezilahabi, 1971: 3).

Suala hilo linamweka Regina katika mitanziko mitatu: mosi, hali ya ndoa yake itakavyokuwa kama atazaa mtoto mwingine wa kike, tofauti na matakwa ya mumewe. Pili, malezi ya watoto wake yatakavyokuwa, kwani atashindwa kutimiza jukumu lake la kuwalea. Kulingana na tamaduni za Kiafrika, jukumu la malezi ya

watoto kwa kiasi kikubwa ni la mama (Momanyi, 1998). Misemo mbalimbali ikiwamo methali isemayo: ‘asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu’ ni uthibitisho wa hili. Tatu, ni kukosa furaha katika maisha yake kwa kosa lisilo lake, kwani, licha ya kumzalia Zakaria watoto watano wa kike, bado anaonekana kupoteza thamani kwake kutokana na kukosa mtoto wa kiume. Mambo haya yanamkatisha tamaa ya maisha kama isawiriwavyo katika Nadharia ya Udhanaishi, na yanamweka katika mtanziko.

### **4.3 Sababu za Kifalsafa**

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1997) inafafanua kuwa falsafa ni taaluma inayojishughulisha na kutafuta ukweli wa jambo kwa njia ya kutafakari. Mantiki iliyomo katika fasili hiyo ni kwamba falsafa ni taaluma au mtazamo unaochunguza matumizi ya dhana, kupima hoja pamoja na mbinu za ujangaji hoja. Mitazamo ya kifalsafa juu ya ukweli kuhusu maisha huweza kusababisha mitanziko kwa wahusika, na hata kwa jamii kwa jumla. Katika riwaya teule, mwandishi anaibua vipengele vikuu vitatu juu ya mtazamo wa kifalsafa kuhusu maisha. Vipengele hivyo, ambavyo ni dhana ya maisha, dhana ya kifo na dhana kuhusu Mungu, vinaibua mjadala na kusababisha mtanziko kwa wahusika kama ifuatavyo:

#### **4.3.1 Dhana ya Maisha**

Dhana kuhusu maisha ni swali linalowashughulisha na kuwatatiza watu wengi wakiwamo wanatheolojia, wanasayansi na wanafalsafa (Muller, 1964). Maelezo tofauti yamekuwa yakitolewa kuhusiana na swali hilo. Kwa mfano, dini mbalimbali zinaeleza kuwa chanzo cha maisha ni Mungu au nguvu zilizo nje ya fikra za binadamu (Mwanzo 1: 26 - 27 katika *Biblia Takatifu*, 1997). Hii ina maana kwamba maisha ya mwanadamu hupangwa na Mungu kutokana na nafasi kubwa aliyonayo katika kuyafanya maisha kuwa kama yalivyo. Aidha, kwa msingi wa dini za jadi za Waafrika, maisha ni mapito kutoka ulimwengu wa kawaida kuelekea ulimwengu wa mizimu (Mbiti, 1969 na Awolalu, 1976). Kwa upande mwingine, wadhanaishi hudai kwamba maisha hayana maana, na wakati mwingine hayapo, kwa sababu ni ya kuwazika tu (Camus, 1954 na Diegner, 2002). Pia, wadhanaishi hupinga kuhusu uwepo wa Mungu na kwamba kila jambo alifanyalo mwanadamu katika ulimwengu wake, hutokana na asili yake tu ya kimaumbile (Camus, 1984).

Kimsingi, kutofautiana kwa mitazamo kuhusu falsafa ya maisha kumesababisha mtanziko mkubwa kwa binadamu; na wengine wameshindwa kabisa kuamini juu ya dhana mbalimbali zinahohusiana na maisha kwa ujumla. Euphrase

Kezilahabi ni miongoni mwa watu wenye mtanziko kuhusu dhana ya maisha. Anadhihirisha hili katika kazi zake mbalimbali. Kwa mfano, katika dibaji ya diwani ya Kichomi (1974: xv) anasema: “Wazo moja hasa lilingumbua. Jambo lenyewe lilikuwa ni swali linalohusu maana ya maisha. Swali hili liliukera sana moyo wangu.” Nukuu hii inaonesha namna Kezilahabi anavyopata mtanziko kuhusu dhana ya maisha. Mtazamo wake kuhusu maana ya maisha kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi unamkatisha tamaa. Hapa anawatumia wahusika kama vile Rosa Mistika, Kazimoto na Manase katika riwaya teule kuendeleza mtanziko wake kwa kuyaona maisha kama kitu kisichokuwa na maana.

Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji*, dhana ya maisha inasababisha mtanziko kwa Manase na Kazimoto. Hawa wanayaona maisha kama kitu kisichokuwa na maana, kwa kuwa hata binadamu mwenyewe anachukuliwa kama kiumbe dhaifu, duni na anayeishi katika ulimwengu usiomjali.

“... mtu yeyote aonaye ngozi hii atafikiri juu ya maisha yake lakini kwa kuwa haoni kitu tena kwa sababu ya woga, polepole ataanza kuona kwamba maisha yake hayana maana. Mnyama kama huyu anaweza kutunyang’anya maisha haya kwa urahisi sana. Kazimoto, kwa ufupi ni kwamba watu wanaoishi katika nyumba hii hawaoni tena maana ya maisha” (Kezilahabi, 1974: 188).

Dondoo hilo linaonesha mtanziko walionao watu waishio katika nyumba ya Manase, kwani hawaoni tena thamani ya maisha kiasi cha kuyafananisha na ngozi ya simba iliyotundikwa ndani ya nyumba yao. Mtanziko wa namna hiyo unaelezwa pia na Mbatiah (1998) anaposema kuwa, maisha ya mwanadamu hayana maana yoyote, ni batili, ya kuudhi na ya kutatanisha. Hivyo, ni dhahiri kwamba mtu anapofikia hatua ya kuona maisha hayana maana, anakuwa katika mtanziko kutokana na kukata tamaa ya maisha yake.

Pia, Kazimoto anapatwa na mtanziko kuhusu dhana ya maisha na anayaona kuwa hayana maana. Matatizo mbalimbali anayopitia yanampa wakati mgumu hasa anaposaili maisha na maana yake. Majadiliano baina yake na Sabina ni ithibati kuhusiana na suala hili:

“Mke wangu,” nilimwita.

“Bwana’ngu,” aliitikia.

“Sijui kwa nini ninaishi.”

“Nimechoka na maswali yako ya kijinga,” alisema.

“Huwezi kuishi kama watu wengine?” Wewe nani?”

“Mimi sijijui,” nilimwambia... (Kezilahabi, 1974: 194 - 195).

Dondoo hili linaonesha namna Kazimoto anavyoyaona maisha kuwa ni adhabu na tanzia kali, ambapo anashindwa kupata njia sahihi ya kujinasua. Maswali anayohojiana na mkewe yanaonesha namna alivyokata tamaa kama isawirivyo Nadharia ya Udhanaishi. Mtanziko wake unamwelekeza katika kujiua kwani anasema hajui kwa nini anaishi na kwamba hajijui.

#### **4.3.2 Dhana ya Kifo**

Dhana ya kifo imemshughulisha sana binadamu kiasi cha kumpumbaza kwa karne nyingi, na kumsababishia mtanziko katika maisha yake (Tempels, 1959; Chuachua, 2016). Mtanziko huo unatokana na kuwapo kwa mitazamo tofauti miongoni mwa watu kuhusu dhana hii. Baadhi huamini kwamba kuna maisha baada ya kifo na wengine hudai kwamba hakuna maisha baada ya kifo. Mbiti (2011) anaeleza kuwa Waafrika huamini kwamba kifo siyo mwisho wa maisha na kuwapo kwa mtu. Anafafanua zaidi kwamba kwa Waafrika kifo ni mwanzo tu wa maisha mengine ya mtu katika ulimwengu wa wafu hai.

Mpalanzi (2019) anaeleza kwamba misingi ya Ontolojia ya Kiafrika inazingatia imani kuwa baada ya kifo, roho za watu waliokufa huendelea kuishi ulimwenguni. Anafafanua zaidi kuwa kulingana na ontolojia hiyo, nafsi ya mtu imejengwa na elementi mbili za msingi ambazo ni mwili na roho, ambapo wakati wa kuzaliwa mtu, mwili na roho huungana. Roho hiyo huendelea kuwapo katika mwili wa mtu katika kuishi kwake. Baada ya mwili kufa, roho huendelea kuwapo ulimwenguni na kuungana na miili iliyo hai.

Kwa ujumla, makala imebaini kwamba suala la kuwapo kwa maisha baada ya kifo, lilikuwapo tangu enzi na lilikuwa na msingi wa imani za kijadi za Waafrika. Kutokana na maelezo hayo imebainika kwamba suala hili limeendelea kupewa msukumo mpya na dini za kigeni zilizoletwa na wakoloni kwa mwavuli wa umisionari. Hata hivyo, kama asemavyo Tempels (1959) kwamba, fikra kuhusu uhai na kifo ni masuala yanayowashughulisha sana Waafrika, makala hii imebaini kwamba ujio wa dini hizo, pamoja na jitihada za kujaribu kuidhoofisha imani ya Waafrika kuhusu suala la kifo na maisha baada ya kifo, haitofautiani na mtazamo uliojengeka katika imani hiyo ya dini za kigeni.

Kwa upande mwingine, Kipacha (2019) anaelezea mtazamo wa wadhanaishi kama vile Nietzsche (1844) na Kezilahabi (1944), wanaonesha mawazo tofauti juu ya dhana ya kifo. Anasema kuwa, wao wanapinga suala la kuwapo kwa maisha baada ya kifo na kuwako kwa uwili wa mwili na roho. Hoja hii inaungwa mkono na Kahigi na Mulokozi (1979) katika Mnenuka (2011) wanapoeleza kuwa, maisha ya



binadamu yanaanza na kuishia hapahapa duniani. Wanafafanua zaidi kuwa, kama ilivyo kwa viumbe wengine, baada ya kufa binadamu huoza na kuwa udongo, na huo ndio unakuwa mwisho wa historia ya maisha yake. Naye Mulokozi (2017), anaona kuwa pamoja na kuwapo kwa fikra za maisha baada ya kifo, maisha hayo ni dhahania kwa kuwa maisha halisi ni ya hapa duniani. Anafafanua zaidi kuwa hakuna pepo wala jehnamu na wala hakuna tunzo wala adhabu baada ya kufa.

Matokeo yanaonesha kuwa katika riwaya ya *Kichwamaji*, dhana ya kifo inamsababishia Kazimoto mtanziko unaotokana na mawazo ya Kalia kwamba mtu akifa huendelea kuishi kwa kuwa kufa ni kubadilika hali. Anasema:

“... Hata! Mara fulanifulani Mungu mpenzi alikuwa anaturuhusu kuja ulimwenguni. Tuliwaona watu, lakini wao walikuwa hawawezi kutuona. Halafu tulirudi. Tulipokuwa tunafika mahali fulani mara hali yetu iligeuka tulikuwa tumezoea kuiita “kupokelewa na Mungu mpenzi.” “Bado sijaelewa, yaani mlikuwa mnatembea kwa miguu?”

“Hapana, tulikuwa tunakwenda tu, hali yetu ilizoea kugeuka na tukajiona mbinguni tena” (Kezilahabi, 1974: 75).

Dondoo hilo linaonesha namna Kazimoto anavyopata mtanziko kuhusu dhana ya kifo. Hii inatokana na mtazamo alionao kwamba mtu akifa hawezi kuendelea kuwa hai tena. Anasema: “Mimi naamini kila kitu kilicho na mwanzo kina mwisho. Na kifo ndio mwisho kwa mwili wa binadamu, roho inabaki lakini haigeuki tena” (Kezilahabi, 1974: 123). Inaelezwa kwamba, baada ya majadiliano yake na Kalia, Kazimoto anajikuta katika mtanziko, huku akifikiria mambo kama vile: mosi, kufa ni kugeuka hali. Pili, waliokufa tuko karibu nao, lakini hatuwezi kuwaona kwa sababu hali yetu haijageuka. Kimsingi, mambo haya yanamweka katika mtanziko, hasa anapoitafakari dhana ya kifo. Kinachojitokeza ni kwamba, Kazimoto anakatishwa tamaa na dhana yenyewe, kwani, licha ya kushindwa kueleweka, bado anaona kwamba mwanadamu hana hiari na uamuzi juu ya kifo chenyewe. Hivyo, anahitimisha kwamba: “Mwisho wa mwanadamu utaletwa na mwanadamu mwenyewe” (Kezilahabi, 1974: 84 - 85). Kwa jumla, kauli hii siyo tu kwamba inaonesha kukata tamaa katika kutafakari juu ya kifo kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi, bali inaonesha pia namna dhana yenyewe inavyomweka katika mtanziko.

### 4.3.3 Dhana kuhusu Mungu

Kuwako au kutokuwako kwa Mungu ni dhana nyingine inayoishughulisha akili ya mwanadamu kwa muda mrefu (Camus, 1954; Awolalu, 1976; Diegner, 2002). Hii

inatokana na ugumu uliopo katika kuielewa na kuielezea dhana hii kwani inahusiana na mambo ya asili na ukweli wa maarifa. Falsafa ya Kiafrika inaeleza kuwa jamii za Kibantu huamini kuhusu uwepo wa Mungu na kwamba ndiye mwanzo wa kuwapo na kuendelea kwa vitu vyote ulimwenguni (Tempels, 1959; Mbiti, 1969; Idowu, 1973). Mathalani, Idowu (1973) anaeleza kwamba katika utamaduni wa Kiafrika, Mungu ndiye kiumbe mkuu na kibainishi cha dini yao. Vilevile, Mungu ni mtawala, muumbaji wa dunia, na chanzo cha kuwapo kwa binadamu. Anafafanua zaidi kuwa katika utamaduni wa Kiafrika, Mungu ni halisi zaidi ya vitu vyote na hutajwa mara nyingi katika sala, hasa wakati wa matatizo. Aidha, *Katekisimu ya Kanisa Katoliki* (1998) inasema: “Mungu ni muumba wa mbingu na dunia, muumba wa watu na vitu vyote na ni Baba mwema.” Kwa upande mwingine, Wadhanaishi wanakana kuhusu uwepo wa Mungu (Nietzsche (1910) kama alivyonukuliwa na Wamitila (2006)).

Suala la ukanaji wa Mungu linajitokeza pia katika riwaya ya *Kichwamaji* kiasi cha kusababisha mtanziko kwa Kazimoto akiwa katika majadiliano na wazee. Mtanziko huo unatokana na mtazamo wake kwamba hakuna Mungu na kukinzana na mtazamo wa wazee hao kuhusu suala hilo. Wazee hao wanakasirishwa na kitendo hicho na wanamwona Kazimoto kama mwehu na mvuta bangi. Mzee mmojawapo anasema:

“Mnazungumza na mwehu!” Alisema kwa kelele. “A! Anasema kwamba hakuna Mungu. Hakuna Mungu! Mtoto wa nani? Mababu na mababu wamekwenda; wamechukuliwa na nani? Bangi!” (Kezilahabi, 1974: 51).

Hapa mwandishi anaonesha kuwa suala la kuamini juu ya uwepo wa Mungu ni gumu, kwani kuna mitazamo inayotofautiana miongoni mwa watu kuhusu dhana hii. Kutofautiana huko ndiko kunakosababisha Kazimoto akose jibu sahihi kuhusiana na kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu. Aidha, Kazimoto anazidi kupata mtanziko anapoambiwa na Manase kwamba Mungu hawezi kufahamika kwa kutumia akili za kawaida. Haya yanajitokeza katika majadiliano baina yao kama ifuatavyo:

“Unafikiri nini juu ya watu wasioamini kwamba Mungu yupo?”

“Ni wajinga,” Manase alisema mara moja.

“Hivi wewe unafikiri mtu asiyeamini Mungu ni mtu gani?”

Nilimuuliza.

“Ni mtu ambaye anataka kumfahamu Mungu kwa kutumia kichwa chake. Mungu hawezi kueleweka kwa akili.”

“Hapo ndipo sikubaliani nawe. Mtu asiyeamini Mungu ni mtu asiyeamua kuwako kwa Mungu kwa kutumia milango ya fahamu peke yake. Licha ya milango ya fahamu mtu asiyeamini Mungu anatumia akili zake. Mimi naona kwamba bongo pia zaweza kukosea.”

“Ndiyo, lakini milango ya fahamu ni zaidi. Ndiyo maana ninasema kwamba lazima vyote viwili viafikiane. Na ndivyo mtu asiyeamini Mungu afanyavyo. Milango ya fahamu ipo kusaidiana na ubongo, lakini bongo lazima zikuchukue nafasi kwanza baada ya kuafikiana.”

“Sioni kwa nini umeingiza ndani mambo ya milango ya fahamu?” Aliuliza.

“Unaona, Manase; mwanadamu ameamua kwamba kuna Mungu kwa sababu ya hali yake ya woga iletwayo na milango ya fahamu. Kwa hiyo, mtu anayeamini kwamba Mungu yupo ni yule aamuaye kwa kufuata milango ya fahamu zake” (Kezilahabi, 1974: 124 - 125).

Kinachojitokeza katika majadiliano hayo ni kwamba Kazimoto yuko katika mtanziko kuhusiana na suala la uwepo wa Mungu. Kauli ya Manase kwamba wasioamini Mungu ni wajinga kwa sababu hutumia vichwa vyao tu ili kumwelewa, inampa wakati mgumu zaidi. Kazimoto anatofautiana naye kimtazamo kwani fikra zake ni kwamba, wanaofikiri kuwa kuna Mungu ni waoga. Hii ni kwa sababu watu hao husukumwa na milango yao ya fahamu tu.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii ilikusudia kuchunguza sababu za mitanziko ya wahusika zinazosawiriwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Kichwamaji* (1974). Mjadala umedhihirisha kuwa mitanziko ya wahusika katika riwaya hizo unatokana na sababu kuu tatu, ambazo ni za kijamii, kiutamaduni na kifalsafa. Kuhusiana na sababu za kijamii imethibitika kwamba suala la mfumo wa malezi na mahusiano ya kimapenzi ni miongoni mwa sababu zinazochangia wahusika kupatwa na mitanziko. Aidha, matokeo yanaonesha kwamba sababu za kiutamaduni zinazotokana na masuala ya mila na desturi, dini, na ndoa na uzazi ni chanzo kingine cha mitanziko ya wahusika. Vilevile, dhana kuhusu maisha, kifo na Mungu nazo ni miongoni mwa sababu za mitanziko inayowakumba wahusika katika riwaya hizo. Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kwamba mitanziko inayowapata wahusika katika riwaya hizo ni usawiri wa maisha halisi ya wahusika wanaokumbwa na mitanziko mbalimbali katika maisha yao. Hii inatokana na ukweli kwamba mtunzi wa kazi ya fasihi, huandika kazi yake kisanaa kwa kuzingatia mambo anuwai anayoyaishi, kuyaona

na kuyasikia katika maisha yake na kuyafikisha kwa jamii yake kupitia kwa wahusika.

### Marejeleo

- Awolalu, J.O. (1976). "What is African Traditional Religion?" *Studies in Comparative Religion*. 10 (2):1-10.
- BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.
- Camus, A. (1954). *The Stranger*. New York: Vintage Books.
- \_\_\_\_\_. (1984). *The Myth of Sisyphus, and Other Essays*. London: Penguin.
- Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Mukadha wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Diegner, L. (2002). "Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early Novels." *Swahili Forum*. 72, IX. Kur. 43-74.
- Faustine, S. (2017). Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya za Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Fuluge, A. (2021). Usawiri wa Mchakato wa Kujiua katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi: Ni Mwangwi wa Mtanziko wa Kijamii?" Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Garofalo, J. (1981). "The Fear of Crime: Causes and Consequences." *Journal of Criminal Law and Criminology*. 72 (2): 839-859.
- Idowu, B. (1973). *African Traditional Religion: A Definition*. Maryknoll: Orbis Books.
- Jimbo Kuu Katoliki la Songea. (1998). *Katekisimu Ndogo ya Kanisa Katoliki*. Songea: Peramiho Printing Press.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.
- \_\_\_\_\_. (1974). *Kichwamaji*. Dar es Salaam: EAPH.
- \_\_\_\_\_. (1974). *Kichomi*. London: Heineman.
- Khamis, S.A.M. (2007). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili." *Kioo cha Lugha*. 5: 13–23.
- Kimani, C. (2003). Suala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi Andishi ya Kiswahili. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Kipacha, A. (2019). Kifo au Maisha ya Maumivu: Usomaji wa *Rosa Mistika* ya Euphrase Kezilahabi kwa Jicho la Kikanushi. Katika A.S. Ponera na Z.A. Badru (Wah.), *Koja la Taaluma za Insia: Kwa Heshima ya Prof. Madumulla* (Kur. 422-434). Dar es Salaam: Karljamer Publishers Ltd.
- Lugano, R.S. (1989). Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia, na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.
- Matteru, M.L.B. (1982). "The Images of Women in Tanzania Oral Literature: A Survey." *Mulika*. 49/2: 16 - 30.
- Mbatiah, M. (1998). "Mienendo Mipya katika Uandishi Mpya wa Kezilahabi: *Nagona na Mzingile*." *Mulika*. 24: 1-11.
- Mbiti, J.S. (1969). *African Religions and Philosophy*. London: Heinemann.
- \_\_\_\_\_. (2011). *African Religions and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.
- Mnenuka, A.J. (2011). "Falsafa ya Maisha katika Ushairi wa Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert." *Kioo cha Lugha*. 9(1): 104 - 121.
- Mpalanzi, L.E. (2019). "Makutano kati ya Dini ya Jadi na za Kigeni: Mifano kutoka Riwaya Teule za Kiswahili." *Kioo cha Lugha*. 17: 114-131.
- Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Muller, R.W. (1964). *The Testament of Samuel Beckett*. London: Faber and Faber.
- Mulokozi, M.M. (1983). "Dunia Uwanja wa Fujjo (Mapitio ya Kitabu)." *Kiswahili*. 50(1): 1-12.
- \_\_\_\_\_. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Musau, P.M. (1995). "Kezilahabi na Thomas Hardy Sarafu ya Pili?" *Kioo cha Lugha*. 1(2): 62-66.
- Ndungo, C.M. (1998). Images of Women in Gikuyu Oral Literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Ogundipe-Leslie, O. (1994). *African Women and Critical Transformations*. Trenton: African World Press.
- Reed, E. (1975). *Women's Revolution: From Matriarchal Clan to Patriarchal Family*. New York: Path Finder Press, Inc.

- Sabinus, J. (2018). Wanaojinyonga Nchini Idadi Yao Inatisha. Katika *Habari Leo* (Novemba) 5:1-2.
- Sletteboe, W. (1997). "Dilemma: A Concept Analysis." Katika *Journal of Advanced Nursing* 26 (3): 449-454.
- Swai, S.O. (2021). *Mirathi Nchini Tanzania: Mwongozo kuhusu Mirathi, Wosia na Taratibu za Kimahakama Tanzania*. Kigoma: Mahakama Kuu.
- Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.
- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wellek, R. na Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. London: Penguin Books Ltd.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books Publications Limited.
- Wamitila, K.W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi, na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni. (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar es Salaam: National Printing Company.
- WHO. (2018). Tanzania ya 27 Afrika Matukio ya Watu Kujinyonga: Katika *Mtanzania* (Januari) 25: 4.